



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA



Kumb.Na. HW/MUH/S.80/14.VOL. II/53

24/12/2025

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza anawatangazia Wananchi wote wa Muheza wenye sifa kutuma maombi ya kazi ya Ukusanyaji wa ushuru wa mazao Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kwa muda wa miezi mitatu (miezi 03) kama ifuatavyo;

1.0 Mkusanya Ushuru wa Mazao (Nafasi 18)

1.1 Sifa za mwombaji:-

- Awe amehitimu elimu ya darasa la saba na kuendelea
- Awe na uzoefu wa kutumia simu janja (Kishikwambi)
- Awe na namba ya kitambulisho cha Taifa (NIDA)
- Awe na uzoefu wa kukusanya ushuru kwa muda usiopungua mwaka mmoja.

1.2 Kazi na majukumu ya mkusanya ushuru wa mazao:-

- kukusanya ushuru wa mazao kwa kutumia mashine ya kukusanyia ushuru (POS) nakuwasilisha fedha hizo benki.
- Kuhakikisha anatumia vitendea kazi vyake vyote vya ukusanyaji wa mapato
- Awe mwaminifu katika utunzaji wa taarifa (data) za serikali
- Kutumia na kuandika takwimu kwenye daftari la ukusanyaji wa mapato ya kila siku.
- kuhakikisha fedha zote zinazokusanywa zinawasilishwa benki kwenye akaunti ya Halmashauri na kutunza nakala ya risiti.

1.3 Ngazi ya Mshahara

Ngazi ya Mshahara kwa kazi hii ni Tshs. 200,000/= kwa mwezi.

BaruazoteziandikwekwaMkurugenziMtendajiWilaya, S.L.P 20, 21402 MUHEZA, Simu: + 027 2977545,
Nukushi: + 027 2977546, Barua pepe: ded@muhezadc.go.tz, Tovuti: <http://www.muhezadc.go.tz>

1.4 Masharti Ya Jumla Kwa Waombaji

- (a) Maombi yote yaambatanishwe na nakala ya vyeti vya kumaliza shule.
- (b) Maombi yaambatanishwe na nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) au namba ya Nida.
- (c) Maombi yote yaambatanishwe na maelezo binafsi ya mwombaji (CV), anuani kamili na wadhamini wawili ambao watatakiwa kuandika barua za udhamini pamoja na namba zao za simu ili kurahisisha mawasiliano.
- (d) Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 29/12/2025 saa 09:30 alasiri
- (e) Waombaji wenye sifa wataitwa kwenye usaili.
- (f) Maombi yote yawasilishwe kwa anuani ifuatayo:

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Muheza
S.L.P 20,
MUHEZA.



Piily M Sindaguru
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI(W)
MUHEZA